Sikika

Jarida la Sikika

Namba ya Usajili - 00005809 Toleo 15: Septemba, 2014

Huduma bora za afya kwa watanzania wote

Mkuu wa Idara ya Rasilimali Watu kutoka Sikika Bw. Zakayo Mahindi akiwasilisha mada juu ya zoezi la Ufuatiliaji na Uwajibijaki kwa Jamii (SAM) katika mkutano baina ya Sikika na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT).

Utangulizi

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka huu (2014), Sikika ilitekeleza shughuli mbalimbali kwa lengo la kuhamasisha uwajibikaji na ufanisi katika upatikanaji na utolewaji wa huduma bora za afya kwa watanzania wote.

Shughuli kuu iliyofanywa na Sikika katika kipindi hiki cha robo ya tatu ya mwaka ni utekelezaji wa awamu ya pili ya zoezi la Ufuatiliaji na Uwajibikaji kwa Jamii – UUJ (Social Accountability Monitoring – SAM) lililofanyika kati ya mwezi Juni hadi Julai katika wilaya tatu za Mpwapwa na Kondoa (Dodoma) pamoja na Singida Vijijini (Singida). Katika wilaya za Mpwapwa na Singida Vijijini, timu za UUJ ziliweza kukamilisha hatua zote 5 za SAM kwa muda, lakini kwa Kondoa kulitokea changamoto zilizokwamisha zoezi hilo.

Kwa ufupi, utekelezaji wa SAM wilayani Kondoa ulisuasua kutokana na ushirikiano duni kutoka kwa uongozi wa halmashauri. Uongozi wa wilaya hiyo, kupitia Baraza la Madiwani ulichukua uamuziwa kusitisha shughuli za Sikika kwa muda usiojulikana, jambo ambalo ni kinyume cha sheria na kanuni za utawala bora. Hata hivyo, Sikika kwa kushirikiana na AZAKI kadhaa zinazojishughulisha na masuala ya kisheria na haki za binadamu zilitoa matamko ya kupinga hatua hiyokupitia vyombo vya habari pamoja na kuwasiliana kwa barua na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa – TAMISEMI, Mh. Hawa Ghasia kumuomba kuingilia kati suala hilo.

Katika kipindi hiki pia Sikika, ilipata fursa ya kukutana na watendaji wakuu wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAOT) ili kubadilishana uzoefu hususani katika kufuatilia matumizi ya fedha za umma kwenye halmashauri pamoja na kufahamu namna ripoti ya CAG katika ngazi ya halmashauri inavyoweza kupatikana kwa urahisi.

Kwa taarifa zaidi kuhusu kazi za Sikika, tafadhali peruzi tovuti yetu; *www.sikika.or.tz*, twitter- *@sikika1*, facebook- *Sikika Tanzania* na blogspot - *www.sikika-tz.blogspot.com.* Kwa maoni tafadhali wasiliana nasi kupitia *info@sikika.or.tz* au sms *0688-493-882*.

Karibu!

Ndani →

Ofisi ya CAG kutumia Ripoti za SAM 2
Ushirikiano duni wakwamisha utekelezaji SAM 3
Kutelekezwa kituo cha afya Mima: Hatua zichukuliwe! 4

Ofisi ya CAG kutumia Ripoti za SAM

Na Gaspar Mashingia, Dar es Salaam

Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali - NAOT imeeleza kuwa taarifa za utekelezaji wa zoezi la Ufuatiliaji na Uwajibikaji kwa Jamii – UUJ (Social Accountability Monitoring – SAM) zinazoandaliwa na Timu za SAM za wilaya, zitasaidia kwenye shughuli za ukaguzi wa hesabu za serikali katika ngazi ya halmashauri.

Mkuu wa Programu Sikika Bw. Patrick Kinemo (Kushoto) akijadili na maofisa kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT) mkoani Dodoma walipotembelea ofisi za Sikika Dodoma ili kujua shughuli mbalimbali zinazofanywa na Sikika.

Kwa mujibu wa NAOT, taarifa hizo zitachangia kupata habari ambazo zitawezesha kufahamu ni maeneo gani yanayotakiwa kupewa kipaumbele wakati wa kuandaa mipango ya ukaguzi katika ngazi ya halmashauri husika. “Kazi zenu zinaweza kutumika kwa kujumuishwa katika mipango yetu ya ukaguzi”, alisema Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Bw. Francis Mwakapalila.

Bw. Mwakapalila alieleza hayo Agosti 2014 jijini Dar es Salaam katika mkutano wa NAOT na Sikika uliolenga kubadilishana uzoefu juu ya shughuli mbalimbali ikiwemo namna ofisi hiyo inavyoweza kunufaika na ripoti za matokeo ya zoezi la SAM. Ripoti zilizotajwa zinatoka kwenye wilaya ambapo Sikika inaratibu mafunzo ya SAM: Iramba, Kiteto, Mpwapwa, Kondoa, Singida Vijijini, Kibaha, Simanjiro, Temeke, Kinondoni na Ilala.

Katika mkutano huo, Sikika ilitoa mada kuhusu tathmini ya utekelezaji wa SAM katika wilaya ambazo shirika linafanya kazi. Vilevile Sikika iliomba kusadiwa kupata ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za halmashauri husika kwa urahisi na kuiomba Ofisi ya Mkaguzi huyo ikubali kuzijumuisha na kuzitumia ripoti za SAM. NAOT ilieleza kwamba taarifa hizo zitachukuliwa kama sehemu ya nyenzo wakati wa ukaguzi wa hesabu za serikali katika ngazi ya halmashauri.

“Tumefurahishwa sana na kazi zinazofanywa na shirika la Sikika na kwa namna yoyote tutatoa ushirikiano wetu katika kazi hii ngumu ya kufuatilia namna serikali inavyotumia fedha. Hii kwa kweli inasaidia wananchi kuwa na uwezo wa kuisimamia na kuiwajibisha serikali yao na mwisho wa siku inafanya shughuli za serikali kuendeshwa kwa uwazi na hivyo kujenga dhana ya thamani ya fedha”, alisema Bw. Mwakapalila.

Naibu Mdhibiti Mkuu huyo alilipongeza shirika kutokana na kazi inazozifanya na kwamba kazi hizo zinasaidia kuwafumbua macho wananchi kuisimamia na kuiwajibisha serikali yao yanapotokea matumizi mabaya ya fedha za umma.

Akifafanua juu ya mafanikio na changamoto wakati wa utekelezaji wa zoezi la SAM katika wilaya mbalimbali, Mkuu wa Programu wa Sikika, Bw. Patrick Kinemo alisema mara kadhaa zoezi hilo lenye lengo la kuhamasisha utawala bora na uwajibikaji wa viongozi limekuwa likikwamishwa na baadhi ya watendaji wa wilaya na hata madiwani. *“Hivi karibuni, shughuli za Sikika zilisitishwa wilayani Kondoa isivyo halali kwa lengo la kuzuia mwendelezo wa zoezi la SAM…pengine mwisho wa siku lingewatia hatiani baadhi ya watumishi wa wilaya wanaofuja fedha za umma,”* alisema Bw. Kinemo.

Katika mkutano huo, Bw. Mahindi Zakayo (Sikika), aliwasilisha muhtasari wa matokeo ya zoezi la SAM katika wilaya za Kondoa, Singida Vijijini na Mpwapwa pamoja na kuelezea mchakato wa SAM na hatua mbalimbali zinazofuatwa katika utekelezaji wake.

Ushirikiano duni wakwamisha utekelezaji SAM

Na Nelson Lema, Kondoa

Utekelezaji wa awamu ya pili ya zoezi la Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii –UUJ (Social Accountability Monitoring - SAM) kwa mwaka 2014 wilayani Kondoa umecheleweshwa kutokana na ushirikiano duni na tuhuma zisizo na ukweli kutoka kwa baadhi ya viongozi wa halmashauri.

Changamoto za SAM zilianza kujitokeza pale halmashauri ilipokataa kuipatia timu ya SAM nyaraka mbalimbali ambazo ni muhimu katika utekelezaji wa zoezi la SAM. Nyaraka hizo ni pamoja na Ripoti ya Utekelezaji wa Miradi ya Afya (2012/2013) na Ripoti ya wilaya ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)-2012/2013. Kitendo hichokinapingana na sheria mama ya nchi, (Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania -1977, Ibara ya 18), inayowapa wananchi haki ya kupatiwa taarifa zinazowahusu.

na kanuni za utawala bora. Baadhi ya viongozi akiwelo Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo pia walitumia mbinu za kuizuia timu ya wananchi ya SAM kuendelea na hatua ya kutembelea vituo vya kutolea huduma na miradi mbalimbali ya afya kwa ajili ya kuhakiki na kuthibitisha taarifa zilizopatikana katika nyaraka walizochambua.

"Kama nia ya halmashauri ni kuboresha huduma za kijamii kwa wananchi wake, ni jambo la kushangaza kuona halmashauri hiyohiyo ikikataa kushirikiana na taasisi za kijamii zinazolenga kuboresha huduma hizo," alisema mmoja wa wajumbe wa timu ya SAM, Bw. Waziri Fataki, "…hatua hiyo inawanyima wananchi haki ya msingi ya kushiriki na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi mbalimbali inayolenga kuboresha huduma za afya kwenye maeneo wanayoishi."

Hata hivyo, Timu ya SAM iliamua kutembelea vituo vya afya wilayani humo bila uratibu wa Sikika. Zoezi la SAM la mwaka 2014 lililenga kuendeleza mafanikio

Mratibu wa Sikika wilayani Kondoa Bw. Nelson Lema (aliyesimama katikati) akizungumza na wananchi katika Zahanati ya Thawi wilayani Kondoa.

Licha ya kukosekana kwa nyaraka hizo muhimu, zoezi la SAM liliendelea kwa kutumia nyaraka chache zilizopatikana ambazo ni Mihutasari ya Baraza la Madiwani (2012/13), Mpango Mkakati wa Halmashauri (2012/17) na Mpango Kabambe wa Afya wa Halmashauri (2012/13). Baada ya kumaliza mafunzo, timu ya SAM ilifanya maandalizi ya kutembelea vijijini/kata ili kujiridhisha iwapo yaliyoandikwa kwenye nyaraka mbalimbali yanaendana na hali halisi.

Wakati maandalizi ya ziara ya timu ya SAM yakiendelea, ndipo uongozi wa wilaya hiyo, kupitia Baraza la Madiwani uliamua kusitisha shughuli za Sikika kwa muda usiojulikana, jambo ambalo ni kinyume cha sheria

yaliyopatikana katika zoezi lililopita (2012) ambapo timu ya SAM ilipata ushirikiano wa viongozi na hivyo kupatamatokeo mazuri hususan kwenye uboreshwaji wa huduma za afya na UKIMWI, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba na rasilimali watu.

Sikika kwa kushirikiana na AZAKI kadhaa zinazojishughulisha na masuala ya sheria na haki za binadamu zilitoa matamko ya kupinga hatua hiyo kupitia vyombo vya habari pamoja na kuwasiliana kwa barua na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mh. Hawa Ghasia kumuomba kuingilia kati suala hilo.

Kutelekezwa kituo cha afya Mima: Hatua zichukuliwe!

Na Aisha Hamis, Mpwapwa

Halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa imekwama kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya cha Mima na hivyo kukwamisha utekelezaji wa azma ya serikali ya kusogeza huduma muhimu za afya karibu na jamii.

Taarifa zinaonesha kwamba takribani shilingi milioni sitini (60,000,000/=) zilizokuwa zimetengwa awali zimeshatumika kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho kilichozinduliwa wakati wa mbio za Mwenge mwaka 2009. Japokituo hakijakamilika wala kuanza kutumika, tayari kimeanza kubomoka hasasehemu za dari na sakafu.

"Mwaka 2012 tuliandika madokezo ya kuomba vifaa ili tuhamishie baadhi ya huduma za zahanati katika vyumba vya jengo la kituo cha afya vilivyokamilika bila kupata majibu kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya," alinukuliwa mmoja wa watoa huduma katika kituo cha afya cha Mima alipokutana na wajumbe wa timu ya SAM ya Mpwapwa iliyotembelea kituoni hapo kwa ajili ya kufuatilia hali ya upatikanaji wa huduma za afya.

Katika ziara hiyo, timu ya SAM ilibaini kuwa kutotumika kwa kituo hicho kumesababisha adha kwa wakazi

Baadhi ya wananchi wakisubiri kupata huduma ya afya katika Zahanati ya Kibakwe wilayani Mpwapwa.

takribani 14,435 wa kata ya Mima yenye jumla ya vijiji vinne (4) vya Mima, Sazima, Igoji 1 na Chamanda. Wananchi hao wanalazimika kusafiri umbali mrefu kufuata huduma mbalimbali zikiwemo za upasuajina kulaza wagonjwaambazo hazitolewi katika zahanati zilizopo kwenye kata hiyo. Zahanati hizo pia zinakabiliwa na upungufu wa watumishi, dawa, vifaa tiba na vitendea kazi.

Hali hii sio tu inarudisha nyuma jitihada za serikali za kuboresha "Afya ya Msingi" bali ni kinyume na haki ya msingi ya binadamu ya kupata huduma bora za afya bila kujali hali zaokiuchumi ama kijamii. Kwa mujibu waMpango wa 'Afya ya Msingi" (2007-2017); serikali imelenga kutokomeza adui maradhi kwa kusogeza huduma za afya zenye ubora karibu na jamii ili kuimarisha ustawi wa maisha na kukuza uchumi wa kipato kwa wanajamii.

Katika kufikia azma hii, serikali imedhamiria kukarabati na kuanzisha vituo vya huduma za afya katika ngazi zote ili kuleta usawa na kuwarahisishia wananchi kupata huduma za afya zinakazokidhi mahitaji yao. Mikakati mingine ni pamoja na kuongeza bajeti kwa sekta ya afya, kuhakikisha uwepo wa watumishi wa afya wenye sifa na ujuzi vituoni pamoja na dawa na vifaa tiba kulingana na mahitaji ya kituo.

Ili kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wa Mima, Sikika inaishauri halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa kumalizia ujenzi wa kituo cha afya cha Mima kwani suala hili liliibuliwa na kutolewa mapendekezo kwa mara ya kwanza na timu ya SAM ya mwaka 2011. 'Kuchakaa'kwa jengo hilo bila kutoa huduma iliyokusudiwa ni hasara kwa walipa kodi, halmashauri na zaidi wakazi wa kata ya Mima wanaosubiri kwa hamu kupatiwa huduma za afya kituoni hapo.

Sikika

Nyumba Na. 69
Ada Estate, Kinondoni
Barabara ya Tunisia
Mtaa wa Waverley
S.L.P 12183
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 26 663 55/57

Ujumbe mfupi: 0688493882
Faksi: +255 22 26 680 15
Barua pepe: info@sikika.or.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz
Blog: www.sikika-tz.blogspot.com
Twitter: @sikika1
Facebook: Sikika Tanzania

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani
S.L.P 1970
Dodoma, Tanzania
Simu: 026 23 21307
Faksi: 026 23 21316